OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA-MKOA WA KAGERA

Namba za Simu: SHULE YA SEKONDARI MUKIRE
Mkuu wa shule: O766825750/0743649715 S.L.P 511
Makamu mkuu wa shule: 0621252815/ 0766256196 KYERWA
TAREHE……

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI……
S.L.P……
……,TANZANIA:

YAH: MAELEKEZO YA KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MUKIRE HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA MKOA WA KAGERA KWA MWAKA WA MASOMO 2022/2023.

1. Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2021 tahasusi ya **HGL** Shule ya Sekondari Mukire ipo umbali wa kilomita 22 **Kaskazini Magharibi ya mji wa Nkwenda-Kyerwa** . Usafiri wa pikipiki, taxi na hiace kutoka mjini Nkwenda unapatikana katika kituo cha mabasi Nkwenda .

   Muhula wa masomo unaanza **tarehe 13/Juni/2022** , hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni **tarehe 13/06/2022**, mwisho wa kuripoti ni **tarehe 30/06/2022**

2. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare ya shule.

a. Sare ya shule hii ni suruali mbili (2) za rangi nyeusi isiyo na michilizi yoyote na yenye mifuko miwili(2) pembeni na nyuma mmoja (1) isiwe “Modal style” Mashati mawili (2) meupe tetroni yenye mikono mirefu. (suruali iwe na miguu yenye “turnups”
b. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visingino vifupi
c. Soksi jozi mbili (2) rangi nyeusi.
d. Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi , usio na madoido.
e. Sare ya michezo ni raba , bukta, tsheti au jezi (Rangi nyekundu aina ya sport yenye michirizi nyeupe).
f. Nguo za kushindia (shamba dress) ni T-shirt za jezi rangi ya bluu mbili zisizo na kola (aina ya sport) Tshirt iwe ya mikono mifupi na isiwe na urembo /mapambo au kudariziwa na suruali mbili damu ya mzee na iwe ya heshima.

ANGALIZO: Nguo nyingine zinapatikana shuleni kwa gharama zifuatazo

i. Sweta Tsh. 14000/=
ii. Tshert Tsh. 10,000/=
iii. Tai Tsh. 3500/=
Michango hii ilipwe shuleni sio bank

2.2 Ada na michango ya shule.

a. Ada ya shule kwa mwaka ni Tsh 70,000/=, unaweza kulipa kiasi cha Tshs . 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja.
- ✓ (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay slip).

b. Michango ya shule

i. Ukarabati wa samani Tsh.15,000/=
ii. Kitambulisho Tshs.6,000/=
iii. Taaluma Tshs. 20,000/=
iv. Ulinzi Tshs. 10,000/=
v. Nembo ya shule Tshs.2,000/=
vi. Matibabu Tshs.20,000/= (Malipo haya hayahusiani na matibabu ya magonjwa sugu na yasiyoambukiza kama kisukari na shinikizo la damu)

vii. Mpishi Tsh.20,000/=
viii. Tahadhari Tshs. 5,000/=
ix. Mock Tsh. 20,000/=
Jumla kuu ya michango pamoja na ada TSHS. 188,000/=

Fedha hii ya michango ilipwe kwenye **akaunti Na. 31901100063 jina la akaunti Mukire secondary School Revenue Collection Benki ya NMB** (Tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye pay slip).

NB. Michango itakayolipwa baada ya tarehe 30/06/2022 italipwa kwa control namba kwa maelekezo yatakayotolewa na ofisi ya mkuu wa shule.

c. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni:

i. Faili mbili – Box file moja na folder file moja (1)
ii. Jembe lenye mpini , panga moja imara , ndoo ya lita 20, hardbroom na softbroom
iii. Ream ya karatasi A4 (kwa mwaka).
iv. Godoro futi $2\frac{1}{2}$ x 6 na chandarua.
v. Mashuka pair 2 ya rangi ya blue bahari na blanketi la rangi yoyote.
vi. Sanduku imara la chuma lenye kufuli.
vii. Sahani ya bati , bakuli, kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula
viii. Ndoo moja (lita 20) kwa ajili kutunza maji na usafi binafsi
ix. Beseni au dishi kwa ajili ya kuogea na usafi.
x. Vifaa vingine vya kutosha vinakubalika shuleni kwa matumizi binafsi kwa muhula mzima.mfano: sabuni, madaftari, toilet paper 5pcs).
xi. Picha .(passport size) 6, 2 za wazazi/ walezi za ndugu wa karibu na 2 za mwanafunzi na namba za simu za wazazi/walezi na ndugu wa karibu 2.
xii. Aje na cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate).
xiii. Mwanafunzi anashauriwa kuwa na vitabu vya tahasusi husika atakayosoma

ANGALIZO.
Fomu zifuatazo zinatakiwa kurudishwa shuleni zikiwa zimejazwa , vizuri,

i. Fomu ya taarifa binafsi za mwanafunzi
ii. Fomu ya kiapo cha kutomiliki simu shuleni
iii. Fomu ya vipimo vya mwanafunzi (vipimo vithibitishwe na Daktari wa Hospitali ya serikali.

2.3 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na. 10 ya mwaka 1995 na 2002.
Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu chini ya ofisi ya Rais TAMISEMI, yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.
Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

i. Heshima kwa viongozi,wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuri ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Night preparation) uwapo ndani na nje ya mipaka wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
iv. Kuvaa sare ya shule wakati wote kwa maelekezo ya sare husika

v. Kutunza mali za umma na za binafsi .
vi. Mawasiliano yasiyo rasmi shuleni.

NB: Siku ya wazazi kuja shuleni ni jumatano tu ya wiki ya mwisho wa mwezi asubuhi saa 4 hadi saa 8 mchana.

2.4 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:-

i. Utoro sugu na kuondoka shuleni bila ruhusa.
ii. Wizi
iii. Uasherati na ushoga
iv. Ubakaji
v. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi ,sigara,ugoro,petrol, cocaine, mirungi , kubeli na kadharika.
vi. Kupigana au kupinga au kuchochea ugomvi.
vii. Kuaribu kwa makusudi mali ya umma
viii. Kuwa mjamzito /kapata mimba/ kusababisha mimba nje na ndani ya shule.
ix. Kugoma kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na nchi.
x. Kukataa adhabu kwa makusidi
xi. Kutembelea nyumba za walimu na jiko la shule bira ruhusa maalumu.
xii. Kufuga ndevu.
xiii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiv. Kuwa na simu ya mkononi au kumliki viashiria vyovyote vya simu ya mkononi.
xv. Kukutwa na vyakula visivyoruhusiwa shuleni.

- **TANIBIHI:** Shule haitoi huduma ya chakula maalumu (special diet) kwa wagonjwa.

2.5 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi (yameambatanishwa nyuma).

i. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
ii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni za maelekezo mengine yatakayotolewa.

2.6 Tafadhari soma kwa makini maelekezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

……..
AMON K.KAIJAGE
MKUU WA SHULE.

OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA-MKOA WA KAGERA
SHULE YA SEKONDARI MUKIRE
S.L.P 511
KYERWA.

3. KUHUSU MWANAFUNZI KUMILIKI SIMU SHULENI.
   Kikao cha bodi ya shule cha terehe 30.04.2021 kilikubaliana na adhabu zifuatazo kwa mwanafunzi atakayekamatwa na simu shuleni:-
   i. Kuchapwa viboko vine 4 mbele ya wanafunzi wote mstarini
   ii. Kusimamishwa masomo siku 21.
   iii. Siku ya kurudi shuleni mwanafunzi atatakiwa kuja na mzazi/mlezi wake na faini ya shilingi laki mbili TSHS. 200,000/= au mizingo mitatu ya seng'enge.

   NB:Endapo mzazi/mlezi atashindwa kutekeleza vipengele tajwa (i-iv) mwanafunzi atafukuzwa shule.

   KIAPO CHA MWANAFUNZI KUTOMILIKI SIMU WALA VIFAA VYA SIMU.
   Mimi (jina la mwanafunzi)……..(jinsi)……
   kwa hiari yangu na nikiwa na siha njema ya akiri naapa kwamba sitomiliki simu ya aina yoyote wakati wote wa masomo yangu ya kidato cha tano na sita . Ikiwa nitakiuka kiapo changu hiki sheria ya Elimu Na 25 ya 1978 itumike dhidi yangu. Pia ninaahidi kutovunja sheria , kanuni na taratibu za shule na za Taifa langu kwa ujumla.
   JINA LA MWANAFUNZI…….. SAHIHI……
   TAREHE……..

OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA-MKOA WA KAGERA
SHULE YA SEKONDARI MUKIRE
S.L.P 511
KYERWA.

FOMU MAALUMU KWA MWANAFUNZI.

1. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI;
   i. Jina la mwanafunzi …….. jinsi……. Tarehe ya kuzaliwa……
   ii. Shule ya Sekondari aliyotoka……
   iii. Jina la baba…….. kazi yake…….. Na.ya simu……..
   iv. Jina la mama……kazi yake…….. Na. ya simu……..
   v. Kijiji /mtaa wanapoishi…….. Wilaya……mkoa ……
   vi. Dini……..
   vii. Majina ya ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kutoa msaada pindi wanapohitajika
      a. …….. Anakoishi…….. Na. ya simu…….
      b. …….. Anakoishi…….. Na. ya simu……
      c. …….. Anakoishi…….. Na. ya simu……
      d. …….. Anakoishi…….. Na. ya simu……
   viii. Michezo anayoweza kushiriki mwanafunzi shuleni
      …… ……. …….
   NB: Je wazazi wote wako hai ? . Ndiyo/ Hapana (Kata isiyositahili)
   Kama amefariki /wamefariki aliyefariki ni……

2. **KUKUBALI NA KUTII SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE**.
   Mimi (jina la mwanafunzi)…….naahidi sitashiriki kabisa katika fujo/migomo na kutenda makosa ya jinai shuleni na maeneo mengine .Pia naahidi kuzifuata taratibu na sheria zote za shule kwa faida yangu binafsi, shule na Taifa kwa ujumla .Endapo nitakwenda kinyume na taratibu na kanuni za shule nakubali kufukuzwa shule, kusimamishwa masomo na kufikishwa mahakamani au kupewa adhabu nyingine kulingana na sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na au sheria ya makosa jinai ya mwaka 2002
   JINA LA MWANAFUNZI…… SAINI……TAREHE…….
   JINA LA MZAZI/MLEZI……SAINI……TAREHE……..

3. **MZAZI/MLEZI KUKUBALIANA NA SHERIA , KANUNI, KULIPA ADA , MICHANGO NA KUTEKELEZA MAELEKEZO YA SHULE.**
   Mimi (Jina la mzazi/mlezi)…….. nakubaliana na sheria , kanuni, kulipa ada na michango yote kwa wakati muafaka na kutekeleza maelekezo yatolewayo na shule. Vilevile , naahidi kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwa uongozi wa shule pindi nikihitajika kuhusu tabia, mwenedo au suala jingine lolote linalomhusu mtoto wangu na maendeleo ya shule kwa ujumla.

   JINA LA MZAZI/MLEZI…… SAINI……..TAREHE…….

……

MKUU WA SHULE.

OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA-MKOA WA KAGERA
SHULE YA SEKONDARI MUKIRE
S.L.P 511
KYERWA.

FOMU YA KUPIMA NA KUJUA AFYA YA MWANAFUNZI.
MGANGA MKUU/MFAWIDHI,
KITUO CHA AFYA/HOSPITALI
……..
……..
……

YAH: <u>KUJUA AFYA YA MWANAFUNZI KWA AJILI YA KUJIUNGA NA SHULE.</u>

Kijana…….. Amechanguliwa kujiunga kidato cha (v) katika shule ya sekondari Mukire.Naomba uthibitishe hali ya afya yake kabla hajaanza masomo rasmi hapa shuleni.
Na endapo atapatikana na tatizo lolote tunaomba utujulishe , na atakapopatikana na tatizo la uoni hafifu hana budi kujinunulia miwani kwa gharama zake mwenyewe.

Kwa
MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI MUKIRE
S.L.P 511,
KYERWA-KAGERA
YAH: AFYA YA……

Nimempima mtajwa hapo juu na kuthibitisha kuwa anasumbuliwa/hasumbuliwi na magonjwa yafuatayo:-

1. TB…….
2. HB……
3. STOOL……..
4. URINE……
5. EYE & EAR'S…….
6. ATHMA…….
7. THYPHOD……
8. OTHER……..

Maoni ya Daktari/Mganga
mfawidhi……
……
……

JINA LA DAKTARI /MGANGA MFAWIDHI ……. SAINI & MHURI ……